**HOTUBA YA MHE. ANTHONY PETER MAVUNDE (MB.), WAZIRI WA MADINI KATIKA MKUTANO WA KIMATAIFA WA MADINI NA UWEKEZAJI TANZANIA WA MWAKA 2023**

**Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

**Waheshimiwa Mawaziri mliopo;**

**Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini;**

**Waheshimiwa Naibu Mawaziri mliopo;**

**Mheshimiwa Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;**

**Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya mliopo;**

**Ndugu Daniel Chongolo, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Taifa;**

**Komredi Abbas Mtemvu, Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Dar es Salaam;**

**Viongozi wote wa vyama vya siasa mliopo;**

**Mheshimiwa Dkt. Mathayo David Mathayo (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na Wajumbe wote wa Kamati mliopo;**

**Waheshimiwa Wabunge mliopo;**

**Bw. Kheri Mahimbali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Madini;**

**Makatibu na Naibu Makatibu Wakuu mliopo;**

**Waheshimiwa Mabalozi mnaowakilisha nchi zenu;**

**Viongozi wa Dini mliopo;**

**Viongozi wote wa Serikali na Taasisi mbalimbali mliopo;**

**Wadau wote wa Mkutano huu,**

DRAFT

**Waandishi wa Habari;**

**Mabibi na Mabwana;**

***"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania"***

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kujumuika pamoja katika Mkutano huiu wa Kimataifa wa Madini na Uwekezaji Tanzania. Nitumie nafasi hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Rais kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika Mkutano huu pamoja na kuwa na majukumu mengi na muhimu katika kulijenga Taifa letu. Aidha, napenda kuwashukuru na kuwakaribisha washiriki wote kutoka ndani na nje ya nchi katika mkutano huu utakaofanyika kwa muda wa siku mbili (2) katika ukumbi huu wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Kama unavyofahamu kuwa, Mkutano huu hufanyika kila mwaka kwa lengo la kukutanisha wadau mbalimbali wa madini kutoka ndani na nje ya nchi ili kubadilishana mawazo, uzoefu na ujuzi kuhusu shughuli za sekta ya madini. Mkutano huu unawezesha wadau wa madini kupata taarifa mbalimbali kuhusu maendeleo ya sekta ya madini. Aidha, Mkutano huu unatoa fursa ya kuhamasisha na kukuza uwekezaji katika Sekta ya Madini kwa kuendelea kuufahamisha ulimwengu rasilimali tulizonazo na utayari wetu katika kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika kuendeleza rasilimali madini tulizonazo. Vilevile, mkutano huu ni sehemu ya kuvutia mitaji ya uwekezaji katika Sekta ya Madini kutoka ndani na nje ya nchi baada ya kuwafahamisha na kutambua fursa zilizopo.

DRAFT

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Mkutano huu pamoja na mambo mengine utawezesha kujadili fursa za uwekezaji zilizopo; upatikanaji wa mitaji; matumizi ya teknolojia ya kisasa na ubunifu katika utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na uongezaji thamani madini kwa kuzingatia uhifadhi na utunzaji wa mazingira. Aidha, Mkutano huu utaangazia masuala ya matumizi ya madini mkakati kwa ajili ya uzalishaji wa nishati safi.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Kauli mbiu ya Mkutano huu ni *"**Unlocking Tanzania's Future Mining Potential**".* Kaulimbiu hii imelenga kuweka mazingira yatakayowezesha kuvuna madini yaliyopo Tanzania kwa manufaa ya kiuchumi na kijamii kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Ili kufikia hatua ya kuvuna madini ni lazima shughuli za utafutaji wa kina wa madini husika ufanyike kwa lengo la kugundua mashapo yanayoweza kuchimbwa kibiashara. Aidha, utafutaji wa madini unakuwa rahisi pale ambapo zipo taarifa za awali za kijiolojia zinazoashiria uwepo wa madini mbalimbali.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Nchi nyingi duniani zilizofanikiwa katika shughuli za uchimbaji madini zimewekeza katika upatikanaji wa taarifa za kijiolojia ambazo hutumika katika utafutaji wa kina wa madini unaowezesha kupata mashapo ya kuanzisha migodi. Upatikanaji wa taarifa za kijiolojia huvutia wawekezaji na wenye mitaji kuwekeza katika utafutaji wa kina wa madini mbalimbali. Tanzania tumejaliwa kuwa na madini mbalimbali ambayo yanatakiwa kuendelezwa kwa manufaa ya ukuaji wa uchumi wa wananchi na Taifa kwa ujumla.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Bado hatujaweza kuwa na taarifa za kutosha za kijiolojia zinazoweza kutumiwa na wawekezaji mbalimbali katika kufanya shughuli za utafutaji wa kina wa madini. Hadi sasa asilimia 16 pekee ya nchi yetu ndiyo imefanyiwa utafiti kwa teknolojia ya kisasa ya *"High Resolution Airborne Geophysical Survey"* ambayo huwezesha kubaini maeneo yenye viashiria vya uwepo wa madini mbalimbali. Kwa kutambua umuhimu wa kupatikana kwa taarifa za kijiolojia, Wizara imejipanga kufanya utafiti wa kijiolojia kwa kutumia teknolojia za kisasa ya *"High Resolution Airborne Geophysical Survey"* ili kuboresha taarifa za kijiolojia zilizopo.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Ili kutekeleza mpango wa upatikanaji wa taarifa za kijiolojia, Wizara imekuja na kaulimbiu isemayo ***"Vision 2030, Madini ni Maisha na Utajiri"***. Kaulimbiu hii inalenga kutumia rasilimali madini kubadili hali ya maisha ya Watanzania kwa kuimarisha vipato vyao kupitia shughuli za uchimbaji wa madini na Sekta nyingine za kiuchumi kufungamanishwa na Sekta ya Madini kwa maendeleo endelevu ya uchumi wa Taifa. Ili tuweze kutumia rasilimali tulizonazo kufikia lengo hilo, tunahitaji kupata taarifa za kijiolojia katika maeneo mbalimbali ya nchi zitakazowezesha kugundua mashapo ya kuanzisha miradi ya madini.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Ili kupata taarifa za kijiolojia, Wizara imepanga kufanya utafiti kwa teknolojia ya kisasa *"High Resolution Airborne Geophysical Survey"* katika eneo kubwa zaidi nchi nzima ifikapo mwaka 2030. Upatikanaji wa taarifa za kijiolojia katika maeneo mengi ya nchi yetu utahamasisha kasi ya uwekezaji katika utafutaji wa kina wa madini nchini ambao ndio msingi mkubwa wa uanzishwaji wa migodi.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Wizara itatekeleza mpango huu kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) na tunafahamu kuwa mpango huo unahitaji kiasi kikubwa cha rasilimali fedha ili kuutekeleza kwa mafanikio. Wizara inaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kuunga mkono juhudi za Serikali katika kufanikisha programu hii.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Tunaamini kuwa, utekelezaji wa Dira 2030 itakuwa ni chachu ya kuongezeka kwa shughuli za utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji, uongezaji thamani na biashara ya madini pamoja na uanzishwaji wa viwanda vinavyotumia madini kama malighafi hususan viwanda vya kuzalisha mbolea, saruji, chuma, *gypsum boards*, nyaya za umeme, chokaa na vinginevyo. Taarifa hizo zinaweza pia kutumika kubainisha maeneo yenye viashiria vya uwepo wa maji ili kufanya utafiti wa kina katika maeneo hayo kwa ajili ya kupata maji yatakayoweza kutumika viwandani, kilimo cha umwagiliaji, wanyama na binadamu. Hivyo, manufaa hayo kwa ujumla wake ndiyo yanayobeba dhana nzima ya kaulimbiu ya **“Vision 2030, Madini ni Maisha na Utajiri”**.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Katika kuhakikisha nchi yetu inanufaika na rasilimali madini, Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta ya Madini ili kuhakikisha inawanufaisha wananchi na Serikali inapata mapato stahiki. Kutokana na usimamizi huo, mwaka 2022/2023 Wizara ilikusanya kiasi cha Shilingi bilioni 678 na inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 882 mwaka 2023/2024 zinazowasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta ya Madini ili kuhakikisha kuwa mchango wake unakua hadi kufikia asilimia 10 ya Pato la Taifa kufikia

DRAFT

mwaka 2025 kama ilivyo katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025. Tutashirikiana na wadau mbalimbali wa sekta kuhakisha lengo hilo linafikiwa.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu,***

Nichukue fursa hii tena kuwakaribisha wageni wetu wote wa ndani na nje ya nchi kwenye mkutano huu muhimu wa sekta ya madini. Karibuni sana Tanzania. Nchi hii ina mazingira bora kabisa ya uwekezaji ikijumuisha jiolojia bora kabisa ya miamba ya madini, mazingira tulivu ya kisiasa na vivutio vingi vya utalii na uwekezaji.

***Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, b***aada ya kusema hayo, naomba sasa nikukaribishe uweze kuongea na hadhira hii pamoja na wadau wengine wanaofuatilia Mkutano huu kwenye runinga na mitandao ya kijamii kutoka sehemu mbalimbali duniani, karibu sana

DRAFT